



The Economic Shield of the Nation

National Investments PLC
50 Mirambo Street
3rd Floor, Mirambo House
P.O. Box 7465
Dar Es Salaam

Phone: +255 22 2111399/ +255 733 006 177

WhatsApp 0733 006 177

E-mail: invest@nicol.co.tz

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI (10) WA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Kumi (10) wa Mwaka wa Wanahisa wa National Investments PLC (NICOL) utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 28 Septemba 2024 kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mkutano utafanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Dar Es Salaam na kwa njia ya Mtandao. Usajili wa Wanahisa utanza saa 2:00 asubuhi.

Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:

- 10.1. MATANGAZO NA AKIDI YA MKUTANO
- 10.2. KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO MKUU WA KUMI (10)
- 10.3. KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA TISA (9)
- 10.4. YATOKANAYO NA MKUTANO WA TISA (9) WA WANAHISA
- 10.5. KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2023
- 10.6. KUIDHINISHA GAWIO LA MWAKA WA FEDHA 2023.
- 10.7. KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI.
- 10.8. KUPITIA NA KURIDHIA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KAMPUNI
- 10.9. KUPITISHA MAREKEBISHO YA SERA YA GAWIO YA KAMPUNI
- 10.10. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2024
- 10.11. MENGINEYO.

MAELEZO MUHIMU:

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano ni lazima wawasilishe nakala ya kitambulisho kama Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mpiga Kura, Pasipoti ya Kusafiria au Leseni ya Udereva.
2. Tarehe ya kufunga Daftari la Wanahisa wanaostahili kushiriki Mkutano itakuwa Jumanne tarehe 24 Septemba 2024.
3. Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura, ikiwa hawezi kuhudhuria kwa sababu yoyote ile, anayo haki ya kuteua muwakilishi kuhudhuria, kuzungumza, na, katika kura ya maoni, kupiga kura kwa niaba yake. Muwakilishi huyo si lazima awe mwanahisa wa Kampuni.
4. Fomu za uwakilishi zitapatikana katika ofisi ya NICOL au kwa kutembelea tovuti ya NICOL www.nicol.co.tz. Fomu ya uwakilishi lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi za NICOL zilizopo Ghorofa ya 3, Mirambo House, Mtaa wa 50 Mirambo Dar es Salaam au kwa barua pepe invest@nicol.co.tz kabla ya saa 10 jioni, siku ya Alhamisi tarehe 26 Septemba 2024.
5. Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kupitia namba zifuatazo: 0733 006 177, 0768 00 88 00 au +255 22 2111 399 na WhatsApp 0768 00 88 00 au 0733 006 177.

Kwa Idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.

Adv. Benjamin Mwakagamba

Katibu wa Kampuni

NATIONAL INVESTMENTS PLC